

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي مَشْرُوعُ تَعَلُّمِ الْإِسْلَامِ – أَحْكَامُ الصَّلَاةِ - سَوَاحِيلِي

Samo la 1

الدرس الأول

HUKMU ZA SWALA.

Swala ni nguzo ya pili katika nguzo za uislamu, nayo ni wajibu juu ya kila muislamu balebhe mwenye akili timamu anawajibika kuitekeleza swala.

Awe amebalebhe kikamilifu kwa kufikia miaka kumi na tano kwa mwanaume, na awe ameshaanza kuota nywele za chini ya kinena (mavuzi) au ameshaanza kutokwa na manii kwa kuota au njenginezo.

Kwa mwanamke ni kufikia umri wa miaka kumi na tano, kuota nywele za chini ya kinena, kutokwa na manii kwa njia ya kuota na kutokwa na hedhi, wakati anapotokewa mtu na vitu hizi basi atambue na kujua kuwa ameshalebhe kafikia umri wa utu uzima.

Yeyote mwenye kupinga swala kwa makusudi basi atambue kuwa amekufuru kwa makubaliano ya wanavyuoni wote, au ikiwa ameicha swala kwa kuipuuza na uvivu basi kwa makubaliano ya maswahaba basi mtu huyo wamesema atakuwa amekufuru.

Swala ndio kitu cha kwanza akacho ulizwa mwanadamu siku ya kiyama kabla ya chochote kile mbele ya Allah. Allah (sw) anasema :

﴿ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا ﴾ [النساء: 103]

(Hakika ya swala kwa waumini ina wakati maalumu) (An-Nisai:103).

Hadith ya Ibn Umar (R.A) bwana Mtume (asw) anasema:

عن ابن عمر رضي الله عنهما ، أن النبي ﷺ - قال: ((بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ: شَهَادَةِ إِلَّا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَإِقَامِ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ، وَالْحَجِّ، وَصَوْمِ رَمَضَانَ)) [متفق عليه: 8 ، 16]

Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudulia ya kwamba hakuna mola anaepasa kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni mwenyezi mungu pekee, na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume wa mwenyezi mungu, na kusimamisha swala, na kutoa zaka, na kuhiji makkah, na kufunga mwezi wa Ramadhan) (Ameipoke Bukhar na Muslim : 8, 16).

Hadithi ya Jabir bin Abdillah (R.A) anasema:

قال رسول الله ﷺ : ((إِنَّ بَيْنَ الرَّجُلِ وَبَيْنَ الشَّرْكِ وَالْكَفْرِ تَرْكُ الصَّلَاةِ)) [رواه مسلم: 82].

(Hakika tofauti iliyopo kati ya mtu, shirki na ukafiri ni kuiacha swala) (Ameipokea Imamu Muslim : 82).

Hakika kutekeleza swala kuna fadhila kubwa sana, miongoni mwa fadhila hizo ni hadithi aliyoipokea Abu Huraira (R.A) amesema : Amesema Mtume (saw) :

عن أبي هريرة رضي الله عنه قال: قال رسول الله ﷺ : ((من تطهر في بيته ثم مشى إلى بيت من بيوت الله ، ليقضي فريضة من فرائض الله ، كانت خطواته إحداهما مَحْطُ خَطِيئَةٍ ، والأخرى ترفع درجة)) [رواه مسلم: 666]

(Mwenye kutawadha nyumbani kwake, kisha akatoka kuelekea nyumba miongoni mwa nyumba zake Allah, atakuwa kila hatua moja apigayo anafutiwa madhambi na nyingine ananyanyuliwa daraja) (Ameipokea Imamu Muslim : 666).

قال ﷺ : ((ألا أدلكم على ما يمحو الله به الخطايا ، ويرفع به الدرجات)) قالوا: بلى يا رسول الله ، قال: ((إسباغ الوضوء على المكاره، وكثرة الخطا إلى المساجد ، وانتظار الصلاة بعد الصلاة ، فذلكم الرباط)) [رواه مسلم: 251].

(Hivi siwajulisheni kitu ambacho Allah anafuta madhambi kwa kitu hicho? Maswahaba wakamjibu kwanini usitulishe ewe Mjumbe wa Allah, Mtume akawaambia: (Nikuufanya vizuri udhu wako, na kuwa na hatua nyingi za kwenda msikitini, na kusubiri swala baada swala nyingine, hiyo ndio ngome na ulinzi) (Ameipokea Imamu Muslim : 251)

في الحديث: ((من غدا إلى المسجد أو راح ، أعد الله له في الجنة نزلاً، كلما غدا أو راح)) [متفق عليه: 662 ، 669].
(Mwenye kwenda msikitini wakati wa asubuhi au wakati wa jioni mwenyezi mungu anamuandalia sehemu ya kufikia peponi, kila anapotoka asubuhi na jioni kwenda msikitini) (Ameipokea Imamu Muslim : 662, 669).